


ZIJUE MBINU ZA KUONGEZA THAMANI YA MAZAO YA MISITU UPATE FAIDA KUBWA ZAIDI

1. Zalisha kwa wingi

- Tenga Msitu Mkubwa wa Hifadhi ya Kijiji. Weka maeneo yote yenye msitu kwenye Hifadhi ya Kijiji "Kijiji kinaweza kufanya biashara ya mazao ya misitu yaliyo katika Msitu wa Hifadhi wa Kijiji tu"
- Wazalishaji wa mazao ya misitu kama mbao, mkaa, samani, na vifaa vingine vya mbao wanashauriwa kuzalisha kwa wingi ili kuvutia wafanyabiashara wakubwa.



2. Wekeza katika matumizi ya technolojia

- Matumizi ya Mashine za kisasa kuchakata magogo huzalisha mbao nyingi na bora zaidi, kwa kutumia miti michache
- Kwa kutumia mashine ya kisasa, Mwaka 2019, Kijiji cha Likawage wilayani Kilwa iliingiza Shilingi za 416,000/=, wakati kwa kutumia msumeno wa mkono, kijiji kingepata Shilingi 260,000/= tu kwa kila mita moja ya Ujazo
- Matumizi ya matanuru ya kisasa huzalisha mkaa mwangi na bora zaidi kwa kutumia miti michache
- Tumia kompyuta au simu yako ya mkononi kutunza kumbukumbu za biashara yako ya mazao ya misitu
- Tumia Mtandao ya kijamii kutangaza bidhaa zako, kutafuta masoko na kuwasiliana na wateja wako.



3. Wekeza katika Mnyororo wa thamani

- Wajasiriamali wadogo waungane ili waweze kuchakata na kuongeza thamani ya mazao ya msitu wa Hifadhi wa Kijiji
- Zingatia kuuza mazao yaliyochakatwa, badala ya kuuza mazao ghafi
- Epuka madalali wasio wa lazima, zingatia kuuza kwa watumiaji wa mwisho kadiri iwezekanavyo



4. Zingatia Mbinu na taratibu za Udhibiti

- Zuia bidhaa haramu za mazao ya Msitu kuzalishwa katika Kijiji chako
- Andaa na tekeleza mpango wa kibiashara
- Epuka gharama zisizo za lazima – mfano safari au vikao visivyo vya lazima
- Epuka migogoro, rushwa na vitendo vingine vya ukiukaji wa sheria ambavyo vinaweza kuongeza gharama zisizo za lazima katika biashara yako



Imeandaliwa na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) kwa Ufadhilli wa Mradi wa Kuongeza Mnyororo wa Thamani ya Mazao ya Misitu Tanzania
Kwa Mawasiliano zaidi: Mkurugenzi Mtendaji; Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA); S.L.P 21522 Dar-es-Salaam – Tanzania; tovuti: www.mjumita.org barua pepe: mjumitaorg@mjumita.org